# HOTUBA YA PROF. GODIUS KAYHARARA KATIBU MKUU WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA KATIKA HAFLA YA KUFUNGA MAONESHO YA 46 YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM, TAREHE 13 JULAI, 2022 KATIKA UWANJA WA MWL. J.K. NYERERE, BARABARA YA KILWA, DAR ES SALAAM

***Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni Rasmi;***

***Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara;***

***Mheshimiwa Omar Said Shaaban (MBW), Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;***

***Waheshimiwa Mawaziri wote mliopo hapa;***

***Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe (Mb.), Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara;***

***Waheshimiwa Manaibu Waziri wote mliopo hapa;***

***Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

***Mheshimiwa Jokate Mwegelo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke;***

***Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu Mliopo hapa;***

***Waheshimiwa Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa;***

***Mwenyekiti na makamu Mwenyekiti wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira;***

***Mwenyekiti na Wakurugenzi wa Bodi ya TanTrade;***

***Bi. Angelina Ngalula, Mwenyekiti na Mwakilishi wa Sekta Binafsi Tanzania;***

***Bi. Esther Mang'enya, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania na wadhamini wakuu wa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam;***
***Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini Mliopo hapa;***
***Viongozi wa Mashirika ya Umma na Binafsi;***
***Menejimenti ya Wizara na ya TanTrade;***
***Ndugu Washiriki wa Maonesho;***
***Wageni Waalikwa;***
***Wanahabari;***
***Mabibi na Mabwana;***

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

**Awali ya yote** ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana leo katika siku hii ya kufunga rasmi Maonesho haya ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ($46^{th}$ DITF) tukiwa na afya njema.

**Pili,** ninayo heshima kubwa kukushukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni Rasmi** kwa kutoa muda wako adhimu na kujumuika pamoja nasi siku ya leo.

Nikushukuru pia **Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara** bila kuisahau Bodi ya Wakurugenzi TanTrade chini ya Mwenyekiti wake **Prof. Ulingeta O.L Mbamba,** kwa

mwongozo na ufuatiliaji wa karibu wa maandalizi ya Maonesho haya. **Asanteni sana!**

Kwa moyo wa dhati kabisa, Napenda kuchukua fursa hii kuishuruku Menejimenti pamoja na wafanyakazi wote wa TanTrade kwa kujitoa kwenu kwa hali na mali ili kuhakikisha Maonesho haya yanakuwa ya kipekee zaidi na tofauti ukilinganisha na miaka mingine. Natambua jitihada kubwa mlizofanya na niwaombe, endeleeni kujituma ili kuijenga zaidi TanTrade kwa ajili ya Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Tanzania na Watanzania kwa ujumla. **Hongereni Sana.**

Sambamba na hili, niwashukuru wadhamini wote mliokuwa bega kwa bega na sisi katika kipindi chote cha Maandalizi ya Maonesho haya. Nawashukuru sana kwa moyo wenu wa kujitolea na niwaombe tuendelee kushirikiana kwa pamoja katika kukuza Sekta ya Biashara nchini.

Nazishukuru pia Kamati za Maandalizi kwa maoni mliyoyatoa na kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Maonesho haya. **Asanteni sana!**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Nipo hapa mbele yenu kwa lengo la kutoa Neno la ukaribisho kabla ya ratiba iliyoko mbele yetu kuendelea, lakini kabla sijafanya hivyo naomba uniruhusu nizungumze machache.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mbali na usimamizi wa Maonesho haya, Wizara imeendelea na majukumu ya kisera ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi ya malighafi zinazopatikana nchini, kuongeza thamani ya bidhaa, kuongeza ajira hususan kwa vijana na wanawake na kuendeleza Kanda Maalum za Kiuchumi na Uwekezaji. Mathalani, katika Maonesho haya pamoja na programu nyingine zilizofanyika, tumeratibu **Programu ya *Total Industrial Solution*** ambapo mitambo mbalimbali inayoweza kukamilisha viwanda vidogo na vya kati imeoneshwa. Hivyo, Mjasiriamali anaweza kumiliki mitambo hiyo inayoanzia thamani ya ***milioni 6 hadi milioni 600.*** Programu hii imehusisha watoa huduma kutoka Sekta ya Fedha nchini wanaowezesha upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali walio na nia ya kuwekeza.

Watembeleaji 230 wameonesha nia ya kununua mashine na mitambo iliyooneshwa ambapo watembeleaji kumi (10) wamepewa Ankara ya Maulizo (Profoma Invoice) kwa ajili ya kununua mashine hizo.

Programu hii itaendelea hapa katika viwanja hivi vya Maonesho kwa muda wa …….. Tutaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wananufaika na programu hii. Hivyo, nitoe rai kwa watembeleaji na Watanzania kwa ujumla kuendelea kufika katika viwanja hivi ili kujifunza na kisha kununua mashine na mitambo hii itakayowawezesha kumiliki viwanda vidogo na vya kati kwa uzalishaji wenye tija.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kama nilivyosema awali, jukumu langu ni kutoa neno la ukaribisho. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kukukaribisha sana katika Maonesho haya na tunashukuru sana kwa kutenga muda wako na kuwa nasi siku ya leo. Nakushukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais.

**Asanteni kwa kunisikiliza!**